**HOTUBA YA MHE. KASSIM M. MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUUWA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA KONGAMANO LA KUMI NAMOJA LA WATAALAMU WA UNUNUZI NA UGAVI (PSPTB) AICC-ARUSHA TAREHE 2 DISEMBA, 2020**

**SALAMU**

- Mheshimiwa Dkt. Philip I. Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango;
- Mheshimiwa Iddi Kimantha, Mkuu wa Mkoa wa Arusha;
- Mheshimiwa Anna Mghwira, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro;
- Mheshimiwa Joseph Mkirikiti, Mkuu wa Mkoa wa Manyara;
- Dkt. Frederick Mwakibinga, Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Wizara ya Fedha na Mipango;
- Ndugu Godfred B. Mbanyi, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB;
- Mheshimiwa Mrisho Gambo (Mb), Jimbo la Arusha;
- Wakuu wa Taasisi zinazoshughulikia ununuzi wa umma;
- Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt. Wilson Mahela;
- Wakuu wa Taasisi za Umma, Sekta Binafsi na Makampuni mbalimbali;
- Mheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Kamati ya Ulinzi na Usalama;
- Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi;
- Wadhamini wa Kongamano;
- Wafanyakazi wa PSPTB;
- Wageni Waalikwa;
- Wanahabari;
- Mabibi na Mabwana.

**Habari za asubuhi!**

**SHUKRANI**

**Mheshimiwa Dk. Philip Isdory Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango,** awali ya yote**,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa uzima na fursa ya kukutana leo katika ukumbi huu wa AICC Arusha.

**Aidha**, nitumie fursa hiikuwashukuru na kuwapongeza wenyeji wetu wa Mkoa wa Arusha mkiongozwa na Mheshimiwa Iddi Kimantha, Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwa maandalizi mazuri ya kikao hiki. **Asanteni sana!**

**Vilevile,** nitumie fursa hii kushukuru kwakunialika kuwa Mgeni Rasmi katika Kongamano la Kumi na Moja la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi. Nimefarijika sana kuwa miongoni mwenu na pia ninawapongeza kwa maandalizi mazuri ya kongamano hili.

**Aidha**, nitumie fursa hiikuipongeza Wizara ya Fedha na Mipango chini ya uongozi wakokwa kuendelea kuisimamia Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) kwa lengo la kuendeleza taaluma ya ununuzi na ugavi nchini.

**Pia,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa washiriki wote wa kongamano hili kwa kutenga muda wenu na kujitokeza kwa wingi kuja kushiriki na kubadilishana uzoefu katika masuala ya ununuzi na Ugavi. Ushiriki wenu ndio mafanikio ya kongamano hili. Najua mmesafiri umbali mrefu salama na tunaomba msafiri salama kurudi kwenye vituo vyenu vya kazi.

**Kipekee,** niungane na wote waliotangulia kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020. Pia, niwapongeze Mhe. Samia , Mhe. Mwinyi na kurudisha salam za pongezi kwenda kwa wote. Ushindi huu mkubwa ni ishara kuwa wananchi wana imani kubwa na kuridhishwa na utendaji kazi wa muhula wa kwanza wa Awamu ya Tano chini ya Jemedari wetu Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Sisi sote ni mashuhuda wa mageuzi makubwa ambayo yamefanywa na Serikali ya awamu ya Tano hasusani katika kuboresha huduma mbalimbali za jamii kama vile afya, elimu, miundombinu, nishati ya umeme na kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kipato cha kati.

**Vilevile,** nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Buhigwe kuwa Mbunge wao na pia kwa Mheshimiwa Rais kukuteua tena kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ni imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais.

**Zaidi ya yote**, napenda kuwapongezawananchi wote wa Tanzania kwa kufanya uchaguzi wa amani na kukichagua Chama cha Mapinduzi kwa wingi wa kura na kukipa nafasi ya kuendeleakuiongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

## MADA KUU YA KONGAMANO LA MWAKA 2020

**Mheshimiwa Waziri,**nimefarijika sana na mada kuu ya kongamano hili ambayo ni ***"Wajibu Wa Wataalamu Wa Ununuzi Na Ugavi Katika Kufikia Ubora wa Juu wa Usimamizi wa Mnyororo wa Ununuzi na Ugavi*"** kwa lugha nyingine "**Reaching Excellence in Procurement Supply Chain and Management)".**

Kama inavyojidhihirisha, mada hiiimejikita katika kutambua wajibu wa wataalam wa ununuzi na ugavi katika kufikia ubora wa juu wa usimamizi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi. Serikali inatambua umuhimuwa taaluma hii kwa kuwa ndiyo wasimamizi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi katika taasisi za umma na hata sekta binafsi.

**Mheshimiwa Waziri,** Serikali inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na kuibua miradi mipya katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Ni dhahiri kuwa pamoja na mambo mengine utekelezaji madhubuti wa miradi hiyo unategemea sana weledi na ujuzi wa Wataalam hawa kwenye manunuzi. Uzembe na ukosefu wa weledikatika kusimamia mnyororo wa ununuzi na ugaviunachangia kukwamisha utekelezaji wa miradiau kufanyika chini ya kiwango na wakati mwingine kutokamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Waziri**, kwa upande mwingine, mada hii inaipa changamoto Bodi yako na wataalam inaowasimamia kuweza kutambua umuhimu wao katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali.Pia, inawapa changamoto ya kuweza kuongeza tija na faida kwa sekta binafsi.

**Kwa mara nyingine,** nitumie fursa hii kuwapongeza kwa mada hii ambayo imesawiri hali na mahitaji halisi ya ugavi na ununuzi. Usimamizi Madhubuti wa mnyororo wa ugavi unahitajika ili tuweze kufanikisha mipango muhimu tuliyojiwekea kama Taifa.

## MWENENDO NA UTENDAJI WA BODI NA WATAALAMU WA UNUNUZI NA UGAVI

**Mheshimiwa Waziri,** kupitia hotuba yako na hata vyombo vya habari mbalimbali kwa nyakati tofauti nimesikia mengi yanayofanywa na Bodi na malengo yanayokusudiwa kutekelezwa katika siku za usoni. Pia nimepata maelezo mengi mazuri ya juhudi na utekelezaji wa shughuli za kukuza taaluma ya Ununuzi na Ugavi. Hii inajumuisha kuongezeka kwa matumizi ya vifaa vya TEHAMA na mifumo ya kielektroniki katika shughuli za kusajili, kudahili na kusimamia wataalamu wa ununuzi na ugavi.

**Aidha**, nimefarijika kusikia wataalamu waliokiuka miongozo na maadili ya taaluma ya ununuzi na ugavi, wamechukuliwa hatua madhubuti za kinidhamu kulingana na mamlaka ya Bodi ikiwemo;

- Kuwafikisha mahakamani wafanyakazi waliokutwa wanafanya kazi za ununuzi na ugavi bila ya kusajiliwa na Bodi,
- Kuwapeleka katika Baraza la Maadili la PSPTB wataalam waliokuwa na tuhuma mbalimbali za kimaadili kwa mujibu wa sheria, pamoja na
- Kuwataka waajiri wazingatie matakwa ya sheria ya PSPTB.

Binafsi ninaipongeza Bodi kwa hatua hii kwani inaongeza umakini katika usimamizi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi na kuleta tija katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Waziri,** pamoja na kutambua juhudi za Bodi na Wizara katika kusimamia weledi na uadilifu kwenye ununuzi na ugavi, lakini upo ushahidi kuwa baadhi ya wataalamu waliosajiliwa na Bodi, uwezo wao wa kitaalamu kusimamia mnyororo wa thamani kwenye ununuzi wa umma unatiliwa mashaka. Hili umelisema kwenye maelezo yako. Aidha, kwa mujibu ripoti ya ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ulibaini kuwa;

- kati ya miradi **131** iliyofanyiwa ukaguzi, miradi **39** ilikuwa na viashiria vya rushwa.
- kucheleweshwa kukamilika kwa miradi kwa wakati, na
- kufanya manunuzi nje ya mpango na bajeti.

Kutokana na ripoti hii pamoja na zile zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni dhahiri kwamba bado tuna jukumu kubwa la kuiimarisha (PSPTB), ili iweze kuendelea kusimamia taaluma hii muhimu kwa maendeleo ya nchi. Pia iweze kuendelea kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali ambazo ni wadau wakubwa kwenye kuhakikisha mnyororo mzima wa manunuzi na ugavi hapa nchini unaleta matokeo chanya kwenye kuimarisha na kukuza uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Waziri,** kwa kuzingatia udhaifu ulioonekana kwenye kaguzi tajwa hapo juu ninaigiza Bodi yako ichukue hatua madhubuti kuinua weledi wa wataalamu na wadau wengine wote wanaoshiriki katika mchakato wa manunuzi na ugavi kwa kuwajengea uwezo katika taratibu za manunuzi na usimamizi wa mikataba na mitaala kutoka vyuoni.

Aidha, iendelee kuchukua hatua za kisheria kwa mtaalam yeyote anayekiuka kanuni za maadili au kutoa ushauri wa ununuzi kinyume na sheria ya manunuzi ya umma.

Kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa maadili kwenye kada hii, iwe chachu kwa Bodi yako kuongeza usimamizi wa maadili na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika kwani taaluma hii ni muhimu kwa Serikali ili kufikia azma yake ya kuendelea kuwaletea maendeleo Watanzania.

**Mheshimiwa Waziri**, napenda kukuhakikishia kuwa Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za Bodi zinazolenga kupunguza au kuondoa kabisa uzembe na ukiukwaji wa maadili katika fani ya ununuzi na ugavi kwani pesa nyingi za serikali, zinatumikakupitia taaluma hii.

**Vilevile,** napenda kutumia nafasi hii kuwaelekeza waajiri wote kutoa ushirikiano kwa Bodi hii, haswa linapokuja suala la usimamizi wa maadili kwa wataalamu waliosajiliwa, kwani hakuna ufanisi bila maadili na weledi. Aidha, ninawataka waajiri wote kuhakikisha wanaajiri watumishi wenye sifa stahiki zinazotambuliwa na PSPTB na kuzingatia mahitaji yaliyopo kwenye Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 3 wa mwaka 2015 wa kada zilizopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

**Pia**, nitumie fursa hii kuwaagiza waajiri wote kuhakikisha wanalipia ada za uanachama wataalam wa ununuzi na ugavi kwani ndio watumiaji wa huduma yao.

**Mheshimiwa Waziri,**nimefarijika kusikia mmeanzisha chama cha wataalam ambapo pamoja na majukumu mengine kitasaidiana na Bodi kusimamia maadili, ufahamu, maarifa na ujuzi ili kuweza kuhakikisha wataalam wote katika sekta ya umma wanazingatia maadili ya taaluma yao. Napenda kuwaasa wanataaluma kwamba fursa ya kutumia utaalamu wao ipo wazi kwani Serikali kwa upande wake imejiandaa kuajiri wataalamu wengi zaidi wenye sifa ili kuiwezesha kupunguza changamoto zinazotokana na upungufu wa wataalamu na inaendelea na jitihada zake za kuboresha maslahi ya wataalamu kadiri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Pamoja na hayo natoa onyo kali kwa wale ambao bado wanaendeleza vitendo viovu kama rushwa, upendeleo, kuingilia michakato ya ununuzi na kadhalika, waache mara moja. Mjitahidi kuwa mstari wa mbele kuepuka vitendo viovu vinavyohusishwa na fani hii ya ununuzi na ugavi. Nawaomba mtambue sheria kali zipo na kwamba Serikali haitakuwa na huruma kwa yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Suala lakutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzikwa muda mrefu ninaahidi nitalisimamia kwa kuongea na mamlaka za uteuzi ili mpate Bodi kwa wakati.

**MASUALA YA MSISITIZO**

**Mheshimiwa Waziri**, manunuzi katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali ni manunuzi zaidi ya **asilimia 70**. Kwa maana hiyo shughuli hii isipofanyika kwa kuzingatia weledi ni dhahiri kuwa wananchi hawataweza kupata huduma iliyokusudiwa na miradi haitatekelezwa kwa viwango kusudiwa. Hivyo, basi yafuatayo ni muhimu kutiliwa mkazo na Bodi. Najua Bodi haijaundwa lakini Mtendaji upo chukua haya, Taasisi pamoja na wataalamu wa manunuzi na ugavi;

i. Bodi isimamie na kuhakikisha wanaofanya manunuzi wana sifa stahiki na lazima watahiniwe ili kuhakikisha wana viwango na maadili yanayotakiwa;

ii. Bodi katika kusimamia weledi wa wataalam wa manunuzi na ugaviihakikishe inafanya kazi kwa umakini, weledi na uadilifu ili kuhakikisha haki inatendeka bila ya uonevu;

iii. Wakuu wa taasisi wote nchini wawatambue maafisa manunuzi na ugavi kwa kiwango sawa na timu ya menejimenti (management level) ili wazishauri taasisi husika ipasavyo;

iv. Taasisi zote zizingatie kutekeleza maagizo ya Serikali ya kufanya manunuzi kwa njia ya mtandao yaani kupitia mfumo wa kisasa wa manunuzi unaofahamika kwa jina la TANePS (Tanzania National e–Procurement System). Matumizi ya mfumo yanasaidia kuongeza kasi ya utekelezaji, uwazi, kupunguza gharama na mianya ya rushwa;

v. Wataalamu wa manunuzi wahakikishe wanatoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi kwa kuzingatia sheria na taratibu za manunuzi ya umma ili kupata matokeo yenye uthamani wa fedha iliyotumika;

vi. Kusimamia vizuri uaandaaji wa mikataba ya manunuzi ili kuepuka nyongeza ya kazi (Variations) na hivyo kuziepusha taasisi katika gharama zilizo nje ya bajeti;

vii. Kuzingatia uwepo wa uwazi katika utayarishaji na utekelezaji wa zabuni ikiwemo kujiepusha na migongano ya kimaslahi au kufuata maelekezo kutoka kwa watu wenye kutaka kufikia malengo binafsi;

viii. Na yale yote yaliyosisitizwa na Waziri wa Fedha. Pia, na suala la Bodi kuisha muda wake.

**MWISHO**

**Mheshimiwa Waziri,** kwa mara nyingine tena natumia fursa hii kukupongeza wewe na menejimenti ya PSPTB kwa kuandaa kongamano hili. Ni matarajio yangu kuwa, maazimio ya kongamano hili yatatoa mwelekeo wa kupunguza changamoto zilizopo kwenye fani ya ununuzi na ugavi. Ninawaahidi kuwa, Serikali ipo tayari kushirikiana nanyi katika masuala yote yanayohusu taaluma ya ununuzi na ugavi.

**Mheshimiwa Waziri,** baada ya kusema maneno haya machache, napenda kutamka rasmi kuwa **Kongamano la 11 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi kwa Mwaka, 2020** limefunguliwa rasmi. Nawatakia kila la heri katika majadiliano yenu na pia msisahau kutenga muda wa kutembelea vivutio vya utalii vilivyosheheni katika jiji la Arusha na maeneo jirani.

**ASANTE SANA KWA KUNISIKILIZA.**